

Press release

Msafara wa Baisikeli Dar es Salaam 2009



Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) pamoja na Chama Cha Baisikeli Dar es Salaam (CHABADA) tunaandaa Msafara wa Baisikeli Dar es Salaam 2009 utakaotokea jumamosi tarehe 24 Oktoba 2009 kuanzia saa mbili asubuhi Uwanja wa Mashujaa, Mnazi Mmoja. Msafara huu utakuwa msafara wa baisikeli wa nne Dar es Salaam – utatokea kila mwaka mwezi wa kumi tangu 2006.

Kwenye Msafara wa Baisikeli idadi kubwa wa wapanda baisikeli wanaendesha baisikeli pamoja kwenye maeneo ya jiji. Siyo mashindano wala mbio na tunaendesha taratibu. Wapanda baisikeli wote wa Dar es Salaam wanakaribisha – vijana na wazee, wanaume na wanawake, wazima na walemavu na baisikeli za aina zote zinakaribisha – baisikeli za kawaida, maguta, baisikeli za mikona za walemavu. Msafara utanza Uwanja wa Mashujaa Mnazi Mmoja, utafuata Barabara ya Bibi Titi Mohammed, Barabara ya Kawawa, Kariakoo na utarudi tena Uwanja wa Mashujaa.

Tunapenda kushukuru mdhamini wetu mkubwa British High Commission. Zawadi za baisikeli tano, baisikeli ya walemavu, helmets 20 na reflecta jaketi 140 zitasambaza kwa washiriki.

Kaulimbiu ya msafara wa mwaka huu ni Mabadaliko ya Tabia ya Nchi (Climate Change). Mabadaliko ya Tabia ya Nchi yanatokea dunia nzima na yanasababisha na utoaji wa carbon dioxide kwenye hewa ya dunia kutoka kuchoma fossil fuels (mafuta, coal, gesi) kwenye viwanda, kwenye magari na ndege na kwenye uzalishi wa umeme. Viongozi wa dunia watakutana jiji la Copenhagen, Denmark mwezi wa Desemba 2009 kukubaliana jinsi ya kuondoa tatizo hilo. Uendeshaji wa baisikeli ni miongoni ya marekebisho ya tatizo kwa sababu baisikeli haitoi carbon dioxide basi ni muhimu kuhamasisha baisikeli kama chombo cha usafiri jijini.

Ili kuhamasisha baisikeli, wapanda baisikeli tunahitaji hali ya barabara iwe salama na nzuri. Kwa hiyo UWABA tunaomba kila barabara kubwa iwe na njia maalum za wapanda baisikeli (kama Barabara ya Nyerere inazo), magari yasitumie service roads kuegesha, kupita foleni wala kuendesha kwa haraka, na sheria za kuepuka uendeshaji wa hatari na mwendo wa spidi zitekeleze vizuri, na barabara ndogo ziwe na matuta kuzuia magari kwenda kwa haraka. UWABA pia tuna mradi wa kufundisha usalama wa baisikeli kwa wapanda baisikeli kwenye jamii na shule.

UWABA tumeona hakuna chama cha siasa hata moja ambacho kimeweka usalama barabarani kwa ujumla au uhamasishaji wa baisikeli kwenye ilani za uchaguzi za mwaka 2005. UWABA tunaita vyama vya siasa kuweka masuala muhimu haya kwenye ilani za uchaguzi za mwaka 2010.

Mashirika

Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)

UWABA ni NGO iliyoanzishwa Januari 2006 na wapanda baisikeli wa Dar es Salaam. Kwa sasa ina wanachama zaidi ya 200, wote wanatumia baisikeli kama vyombo vya usafiri wa kila siku hapa Dar es Salaam. Malengo ya UWABA ni kuhamasisha baisikeli kama vyombo nzuri wa usafiri Dar es Salaam, kuhamasisha serikali kuboresha usalama na mazingira kwa wapanda baisikeli, kulinda haki za wapanda baisikeli, kuhamasisha waendesha gari kuheshima wapanda baisikeli na kuelimisha wapanda baisikeli kuhusu usalama barabarani. UWABA tunakutana kila jumamosi saa nne asubuhi kwenye ofisi yetu Manzese Sisi kwa Sisi. Taarifa zaidi inapatikana kwenye tovuti yetu www.uwaba.or.tz au kwa simu kwa mwenyekiti Mejah Mbuya (0713652642) au katibu Elaine Baker-Guni (0715568512 / 0754568512).

Chama cha Baisikeli Dar es Salaam (CHABADA)

CHABADA ni shirika la Dar es Salaam linaloshughulika na michezo na mashindano ya baisikeli. Ilianzishwa mwaka 1975 na ina wapanda baisikeli 70 wanaofanya mazoezi kawaida. Inafanya kazi pamoja na shirika la taifa la michezo ya baisikeli CHABATA. Wanashughulika na michezo ya baisikeli Dar es Salaam, wanahamasisha matumizi mazuri ya baisikeli na inafanya mazoezi ya baisikeli. CHABADA wanakutana kila jumapili kufanya mazoezi ya baisikeli. Kwa taarifa zaidi wasiliana na katibu mkuu Saidi Kengelle (0754 314341) au technical supervisor Godfrey Jax (0717 009751).